MWONGOZO KWA MWEZESHAJI
JINSI YA KUENDESHA KUNDI LA WALENGWA LENYE WATOTO
"ACHA UBAGUZI NA UGANDAMIZAJI DHIDI YA WASICHANA"

Je umewahi kuongoza mjadala na kundi lolote la walengwa? Pata 'ABC' kwa kifupi mwongozo wa jinsi ya kufanya.

Kwa ujumla unaweza kuhitaji siku tatu kamili ili kuandaa, kuendesha mjadala na kuripoti kuhusu somo uliloendesha kwa kikundi cha walengwa. Hii itajumuisha kukubaliana pamoja na walengwa waalikwa, na washiriki, juu ya tarehe, muda na mahali, sanasana, wiki moja au zaidi kabla ya muda.

A. Ili Kujiandaa kuongoza kundi hilo la walengwa unahitaji:

1. Kujizoesha kusoma mara nyingi majarida ya Toleo Rafiki la Vijana la ripoti ya EGM. Jisikie huru na yaliyomo na maswali yanayoulizwa, jaribu kuvutika na kuyajibu mwenyewe – fikiria wigo wa mila na desturi za nchi uliopo – fikiria juu ya sifa za kundi la walengwa unalotarajia kukutana nalo.
2. Ukikuta swali lolote linalohitaji maelezo zaidi ya ilivyo kwenye makala, itabidi uzuipange habari hizo nakupata jawabu mapema ili ikusaidie kuelezea swali.
3. Ainisha vigezo vya kuchagua washiriki wa kikundi cha walengwa. Je wanatokea katika mradi, programu, je wanatoka katika mazingira yanayofanana na rika sawa? Je utahitaji kupanga kupata msaada wowote wa watu wazima kumsaidia mshiriki ili kufuatilia vizuri mada inavyojadiliwa, ambae huenda akawa na athari za kisaikolojia – ni nani watakaokuwa wasaidizi?
4. Tunapendekeza ujihusishe na uliongoze kundi la walengwa lenye vijana wa umri kati ya miaka 10 – 18, lakini lililogawanywa katika makundi mawili, miaka 10 – 13, na 14 – 17, ili washiriki wawe katika kiwango sawa.
5. Unapaswa kuzingatia umri na jinsia ya kila mshiriki atakayejumuishwa katika ripoti ya mwisho.
6. Kwasababu baadhi ya masuala yanayojadiliwa yanaweza kuonekana nyeti, inashauriwa wasichana na wavulana kutenganishwa katika makundi yakijinsia.
7. Kama kundi ni la wasichana inashauriwa mwezeshaji awe mwanamke, na kwa kundi la wavulana na awe mwanaume.
8. Unapaswa kujiandaa kuliongoza kundi la walengwa lenye vijana 6 – 10; makundi madogo ni mazuri zaidi kuyamudu kuliko makundi makubwa. Sehemu ya wajibu wako ni kuona na kuhakikisha washiriki wote wanapatafursaya kuelezea maoni yao.
9. Kama kundi la walengwa linajumuisha wasichana dhaifu, rahisi kuathirika, itakubidi kufikiria njia nzuri ya majadiliano ya moja kwa moja badala ya kuwajumuisha kwenye kikundi. Utaweza pia kumwalika mtu mwingine atakaeweza kutoa msaada wa nyongeza kwa msichana alie katika hatari, kabla, wakati na baada ya mashauriano (mf. Afisa mradi au program ambaye tayari anafanya kazi na wasichana).
10. Ni jukumu lako kuelezea yaliyomo kwenye waraka. Tukitarajia kwamba utaliongoza kundi la tarajiwa lenye wasichana (na wavulana) walio katika mazingira hatari utahitaji sana kuuelezea waraka kwa kutoa mifano iliyo

rahisi kwa vijana kuielewa na inayohusiana. Hii itajumuisha kuonyesha michoro Fulani au kutumia vifaa vingine husika viatakavyorahisisha uelewa wa mada.

11. Kumbuka wajibu wako ni kuwawezesha washiriki kujiamini ili waweze kuelezea maoni yao. Jaribu iwezekanavyo kutoegemea popote. Jaribu kutohuku au kuruhusu tofauti ya maoni kutokea. Wakati huo huo, hakikisha washiriki wanaheshimiana na kujisikia huru na salama kuongea kwa uwazi. Fikiria jinsi utakavyoelezea vitu kabla ili kuepusha jazba na maneno ya kuhukumu epuka misemo ambayo itaweza kuwaudhi washiriki. Kumbuka utahitaji kupanga kwa kina jinsi utakavyotumia muda wako ukiwa na kundi la walengwa; hii ni pamoja na kujua urefu utangulizi, utauliza maswali mangapi, na walau mara ngapi utahitaji kuingilia kati, ni vipi utahakikisha washiriki wanapata nafasi ya kutoa maoni yao, ni kwa jinsi gani utatamatisha na ni nini washiriki wanatarajia kukipata kutoka kwako? Je utajuaje muda muafaka wa kuingilia kati?

B. Kuendesha mjadala kwenye kundi la walengwa unahitaji:

1. Kuhakikisha kwamba mamlaka ya pale pale (viongozi wa jamii, wazazi, walezi, waalimu, viongozi wa dini, meneja wa azimio au mradi wamejulishwa na kukubali kuacha vijana wa jamii yao au kikundi washiriki) kana kwamba ni yenye maana kwa usalama na ukamilifu wa washiriki.
2. Mahali penye ukimya na pasipokuwa na usumbufu pakukutana pamoja na kikundi cha walengwa cha washiriki. Kwa mfano: Chumba ambapo mnaweza kukaa katika mfumo wa duara, chini ya mti kivulini, mbali na kelele au mkusanyiko mkubwa wa watu.
3. Msaidizi, ambae atakusaidia kunakili na kumorodhesha yule ambae angependa kuzungumza au kama utamtambua mtu mapema.
4. Kugundua kama mnaweza kuwasiliana moja kwa moja (inapendekwa)aukama unahitaji kumtumia mkalimani, kama ndivyo hivyo mtu huyu atajumuishwa pamoja na msaidizi. Kama utahitaji kuwasiliana kupitia mkalimani unapaswa kujizoesha nae na ni lazima uwe wazi kanakwamba yeye asionekane kuwa ndio mwenye kuvutwa kwa urahisi au wenye kuongeza maoni yao binafsi; hili ni muhimu sana ili kuweza kupokea habari za kweli. Hakikisha mkalimani wako wa kutokea hapo anakubalika kwenye kikundi cha walengwa(kama wewe ni mwanamke mwendeshaji wa kundi la walengwa la wasichana mkalimani wako pia anahitaji kuwa mwanamke au msichana).
5. Tumia kinasa sauti ili uweze kuorodhesha ujumbe wote na uwazingatie vijana ambao unawahoji.
6. Lazima uelezee mwanzoni na mwishoni nini dhumuni kwa kundi la walengwa na kuwahakikishia washiriki wote kwamba, taarifa binafsi za hakika zitakuwa siri. Weka taratibu kwa ajili ya kikundi na washiriki, kwa mfano anapaswa kunyanyua mkono wake na kupata ishara kutoka kwako ya kumruhushu kuongea.
7. Kumbuka jukumu lako ni kuelezea na kuuliza maswali, na sio kutoa maoni yako. Unatakiwa kugundua njia tofauti za kuelezea swali hilo hilo kuhakikisha kwamba washiriki wote watakuelewa vizuri.
8. Watazame washiriki, hakikisha unahamisha usikivu wako kati ya washiriki wote, na hakikisha unashirikisha kila mmoja.

9. Andaa vichekesho vya kutumia kuwafanya washiriki waburudike na wajisikie furaha na kuvutiwa na kile wanachokifanya.
10. Walengwa watakaa popote mkao mmoja kati ya dakika 45 hadi lisaa na SI ZAIDI ya lisaa na nusu, vinginevyo halikubaliki!
11. Hakikisha mwishoni unatamka tena dhumuni na kwa habari ambazo washiriki wamekupatia zitatumika. Uwajulishe kama utarudi na ushirikiane nao yale matokeo, ya kawaida, ya kitaifa na kimataifa ambacho hili kundi la walengwa limechangia. Kama hunauhakika namna nini utakachorudi nacho, usiahidi ambacho huwezi kutekeleza.

C. Ili kutengeneza ripoti kutoka kundi la walengwa ulilioongoza unahitaji:

1. Kurekodi jina la kwanza, umri na jinsia ya kila mshiriki wa kikundi.
2. Mara tu umalizapo kuendesha mjadala na walengwa andika hisia zako (je kulikuwa na muitiko mwema katika kikundi? Je palikuwa na vipengele vingi vinavyopingana? Je kila mmoja alikubaliana? Je wote walishiriki sawa au baadhi ya watu walishiriki zaidi ya wengine? Je ulikuwa mjadala hai unaovutia au je ulikuwa mjadala butu usio endelevu?). Na kama iwapo msaidizi au mkalimani alitumika, je waliingiza fikra zao.
3. Na je huyu msaidizi wako amehitimisha muhtasari wake kutokana na mjadala wa walengwa?
4. Andika chini dondoo na kinasa sauti.
5. Anza kwa utangulizi mfupi, ukizingatia tabia, idadi ya washiriki, umri, jinsia, kiwango cha elimu, hali ya maisha, eneo la kijiografia wanaloishi uhalisi wake au isiyo halisi, ikibidi, tumia majina bandia kwa usalama na kulinda hadhi za washiriki.
6. Elezea maswali yalioulizwa (yaorodheshe) na majibu. Jaribu kutenganisha miitiko na majibu katika sehemu nne ya ripoti ya kirafiki juu ya vijana, ukitumia dondoo kusaidia kama kudhihirisha kile ambacho kimeelezwa.
7. Orodhesha lolote kuu unaloligundua na mahitimisho yako.
8. Jaribu kuweka ripoti yako isizidi kurasa 5 kwa upeo.
9. Tafadhali andika ripoti yako kwa Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi, Kihispania au Kiswahili.
10. Tutumie ripoti yako kabla ya tarehe 15 Januari 2007 kupitia njia hizi tatu:
    - **Tovuti**: Ingia kwenye Sauti za Vijana (http://www.unicef.org/voy/) na ubonyeze kwenye "Acha Ubaguzi na Ugandamizaji dhidi ya wasichana" kujibu maswali katika tovuti.
    - **Barua pepe**: voy@unicef.org, pamoja na kichwa cha habari "Acha Ubaguzi na ukandamizaji dhidi ya wasichana".
    - **Kwa Barua**: Voices of Youth, 3 UN Plaza, New York City, NY 10017, USA.

Sasa kwa vile umeshapitia hizi 'ABC' uko tayari kuanza:

NAWATAKIA MAFANIKIO KATIKA BARAZA NA KIKUNDI CHA WALENGWA!